Toleo 2

# Ukweli Wa Injili

*Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote*


## HAMNA WOKOVU KUTOKA KWA MTU MWINGINE AWAYE YOTE

Machozi yalitiririka usoni mwa kijana huyo huku akijipiga viboko kwa mjeledi kwa sababu ya dhambi zake. Mahali kwingine ulimwenguni mama mmoja kizee mwenye uso uliokunjamana alipiga magoti mbele ya sanamu na kupeana pesa zote alizokuwa nazo. Nako mahali kwingine babu mmoja alikuwa akitembea kwenye barabara ndefu iliyojaa vumbi huku akifanya safari ya kidini ili kufika mji mtakatifu kabla ya kifo chake.

Wakati huo huo mwanadada mmoja kijana alipiga magoti mbele ya sanamu takatifu na kufanya maombi ili aweze kupata rehema kabla ya kufanya toba yake kwa kuhani ambaye aliyekuwa amevaa mavazi meusi. Na katika mji jirani maombi yalisikika kote kwenye mji huo huku halaiki ya watu wakilala sakafuni kifudifudi.

Nako katika bara lingine (la mbali) kijana mmoja ambaye alikuwa nadhifu na mke wake pamoja na watoto wao wawili waliwapatia maskini waliokuwa hapo supu ya kunywa. Na huko upande mwingine wa barabara msichana na mvulana ambao hawajaoana waliendelea kunywa pombe na kushibisha tamaa zao za mwili.

Ngoma ziliendelea kupigwa kwa sauti ya juu huku kijana huyo mdogo ambaye alikuwa amepagawa na mapepo akitupiwa damu na maji. Na katika chumba kimoja katika nchi ya mbali baba mmoja alifanya miguu yake kupitana huku akitafua amani na usalama kupitia kwa tafakari aliyokuwa akifanya.




Katika nchi nyingine moshi ulipanda kutoka kwa kafara ambayo ilikuwa ikichomwa kuwafurahisha miungu ili walete amani kwa wenye kufanya ibada. Na huko katika umbali wa maelfu ya maili msichana mmoja alitembea katikati mwa viti vya kanisa ili kumsalimu mhubiri. Hata ingawa watu hawa wote walikuwa katika nchi tofauti na wenye imani tofauti na mazoea tofauti wao wote washiriki kitu kimoja kwa pamoja—walikuwa watafutaji wa amani, furaha, kutosheleka, na uhai wa milele.

Kwa kawaida watu hujitegemea wao wenyewe, hutegemea matendo yao mema, hutegema anasa za mwili, hutegemea makuhani au manabii, hutegemea wahubiri, hutegemea sadaka zao na misa zao, hutegemea hata kanisa au matamko ya kidini, n.k. huku wakijaribu kuziba pengo lililoko rohoni mwao. Wao wanatafuta wokovu lakini wengi wao hata hawajui shauku la mioyo yao ni nini.

Lakini wokovu haupatikani kwa yeyote yule isipokuwa kwa Yesu aliyesulubiwa: “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo 4:12).

Watu wanaweza kutafuta ulimwenguni kote na kutoa vitu mingi kama sadaka, lakini utafutaji huo wote wao hautafaa chochote hadi watakapoliitia jina la Yesu Kristo – Mwana wa Mungu Aliye Hai. ■


Hamna Wokuvu Kutoka kwa Mtu Mwingine Awaye 1

Je, Nifanye Nini Ili Niweze Kuokoka? 3

Somo la Bibilia: Dhambi 4-5

S & J: Je, Mkristo Anaweza Kuishi bila Kutenda Dhambi? 6-7

Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

# Mambo Yenye BIBLIA Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Petro 1:20-21, Mat. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mat. 22:37-40, Yohana 14:21-23, 1 Yohana 4:7-21
**Toba**
Matendo 3:19, 17:30, 2 Kor.7:10
**Uzao Mpya**
Yohana 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rumi 6:1-4, Efeso 2:1, 5-6
**Uhuru Mbali na Dhambi**
1 Yohana 5:18, Mat. 1:21, Yohana 8:11.
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Matendo 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Waebrania 12:14, 1 Petro 1:15-16, Tito 2:11-12, Rumi 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Luk. 17:20-21, Rumi 14:17, Yohana 18:36
**Kanisa**
Matendo 2:47, Efeso 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yohana 17:20-23, Wagaltia 3:28, Ufunuo 18:2-4.
**Kumbukumbu**
Mat. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yohana 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isaya 53:4-5, Yakobo 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mat. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11.
**Mavazi ya Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, K. Torati. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Petro 3:7-12, Yohana 5:28-29, 2 Kor.5:10, Mat. 25:31-46
**Kutojipigania**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yohana 4:23-24, Efeso 5:19, 2 Kor. 3:17
**Mwito Mkuu**
Marko 16:15

# Tahariri



Moyo wangu umejaa shukrani kwa ajili ya kuokolewa kutokana na dhambi kupitia kwa damu yake Yesu Kristo. Wokovu ambao niko nao leo haukutokana na wema wowote ndani yangu bali ulitokana na rehema zake Mungu. Lakini ujuzi huu wa kibinafsi wa wokovu wa Mungu ni zaidi ya mtu kufanya tafsiri zinazofaa za maandiko na hata ni zaidi ya thiolojia ya wokovu. Mimi hupata amani ya ajabu ninapoenda kulala kila siku huku nikijua kwamba dhambi zangu zimesamehewa na kwamba mimi ni mtoto wake Mungu. Kuna uhakikisho mkubwa ambao hauotokani na uwezo wangu wa kibinafsi bali unatokana na nguvu za kuokoa na kudumisha za Mwokozi wetu Yesu Kristo. Shauku langu na mzigo ambao niko nao ni kwamba somo la robo hii ya mwaka ambalo linahusiana na swala la wokovu na dhambi litaangazia mioyo na akili za watu ili wapate kujua ujuzi wa wokovu na pia liangazie mafundisho ya uwongo ambayo yamesambaa sana katika ulimwengu wa sasa kuhusiana na swala la wokovu.

Mimi nafurahia ukweli kwamba sasa gazeti hili linatafsiriwa kwa lugha ya Kihispania na Kiswahili. Sisi pia tunamtazamia Bwana ili atupatie watafsiri wa lugha ya Chichewa na lugha zingine. Himizo langu ni kwa wafanyi kazi wenzangu katika Injili nikiwaomba kupigana vita vizuri vya imani. Kwa kweli vita ni vikali lakini ushindi ni wetu kupitia kwake Yesu Kristo. ■


## UKWELI WA INJILI

Gazeti la Ukweli wa Injili huchapishwa kwa jina la Bwana kwa ajili ya watu wote wa mataifa yote kwa kusudi la kuwapatia msingi bora na kuwahimiza watu wa Mungu kupitia kwa ukweli wa Neno la Mungu. Gazeti hili hufunza na kupigia debe kweli za Biblia ambazo zimekuwako tangu wakati wa Yesu na mitume.

Neno la Mungu ndilo msingi wa pekee wa imani ambayo inakubalika na ambayo sisi tunaamini. Neno hilo linafundisha kuhusu wokovu na ukombozi kutoka dhambini kupitia kwa utakaso wa Yesu Kristo; na hapo baadaye mtu hujazwa Roho Mtakatifu ili amwongoze, amuonyeshe njia, na pia kumpatia nguvu. Wokovu huo pia unahusiha mtu kuwa na utakatifu wa vitendo katika kila fani ya maisha yake; na pia kuhusisha umoja na ushikamano wa watu wa Mungu. Huduma ya Mungu ambayo inakubalika ni kwa mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na Yeye, uhusiano ambao ni wa upendo na ambao msingi wake ni ukweli. Wahariri: Michael na Rene Smith

## JIANDIKISHE ILI UPATE NAKALA YAKO

Ukweli wa Injili ni gazeti la kielektroniki ambalo litachapishwa kulingana na mwongozo wa Bwana. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili ujiandikishe kupata notisi ya kupokea nakala zitakazokuwa zikichapishwa. Hebu jisikie huru kutumia mhariri wa gazeti hili orodha ya majina na anwani pepe za wale ambao wangependa kupokea toleo hili.

## ANWANI

Ukweli wa Injili huchapishwa katika nchi tofauti tofauti ili isambazwe katika nchi hizo. Yeyote ambaye anataka kuunga kazi hii mkono anaweza kutuma msaada wake kupitia kwa ofisi hii. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo zinafanywa na ofisi hii zinaungwa mkono na matoleo ya hiari ambayo hutolewa kwa jina la Kanisa la Mungu. Ukitaka unaweza kuomba upewa risiti kulingana na jinsi tumelipa ushuru kutokana na matoleo yako ya kifedha.



Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA

editor@thegospeltruth.org

# WOKOVU

JE, NIFANYE NINI ILI NIWEZE KUOKOKA?

## Hatua za Kimsingi

**I. AMINI –** *mtu kuwa na imani au kuamini kitu; kukubali kwamba jambo fulani ni la kweli, kuwa mkweli, halali.*

Matendo 16:30-31 Kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.

Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Warumi 10:9 Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.

**II. KUITA** – *kuomba; kuuliza upewe*

Warumi 10:13 Kwa kuwa, kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.

**III. KUKIRI** – *kutangaza au kujulisha, kukubali waziwazi.*

Warumi 10:10 Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

Mithali 28:13 Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.

**IV. KUTUBU** – *kuachana na; kubadilisha kauli; kuhisi majuto kwa ajili ya matendo ya mtu, majonzi au kujihisi vibaya kutokana na matendo ya mtu.*

Matendo 3:19 Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana.

2 Wakorintho 7:10 Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.

Isaya 66:2 . . . lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu.

**V. POKEA** – kukubali; kuruhusu kitu kuingia ndani yako.

Yohana 1:12 Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.

### Ombi la Mwenye Dhambi



*Ewe Yesu, ninaamini kwamba wewe ni mwana wa Mungu na kwamba ulikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu. Naomba tafadhali unisamehe na kunitakasa kupitia kwa nguvu za damu yako iliyomwagika. Ninakupokea kama Mwokozi wangu wa kibinafsi na ninakukaribisha moyoni mwangu. Ninatubu na nitaachana na maisha yangu ya dhambi. Asante kwa kusikia ombi langu na kwa kuniokoa kupitia imani katika jina lako. Asante kwa kipawa cha uzima wa milile. Ninakutukuza na ninakwabudu kama Bwana wa maisha yangu.*

*-Amina*

## Hatua Zinazofuata

**I. KUBATIZWA** – *tamaduni ya kumtumbukiza mtu majini mwili wote kama ishara ya yeye kuoshwa dhambi zake na kuzaliwa tena ndani ya Yesu Kristo.*

Matendo 2:37-38 Tubuni mkabatizwe kila mmoja.


Mathayo 28:19 Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.

**II. KURUDISHA** – *kitendo cha kumrudishia kitu yule ambaye ni mwenyewe kwa haki, kurudisha kile ambacho kilikuwa kimechukuliwa, kimepotea, au kilichosalimishwa.*

Luka 19:8-9 Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne.

**III. SAMEHE** – *kusamehe makosa; kuachana na chukizo linalotokana na kufanyiwa makosa; kuacha kudai adhabu kutolewa kwa makosa uliyofanyiwa*.

Marko 11:25-26 Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni.



**Warumi 6:13-18**

*Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.*

*Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.*

*Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha!*

*Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.*

*Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake;*

*Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.*

# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## SOMO : DHAMBI

### I. Chanzo cha Dhambi

A. Warumi 5:12 Kwa mtu mmoja dhambi ikaingia ulimwenguni.

B. Warumi 5:19 Kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi.

### II. Kiasili Mwanadamu ni Mwenye Dhambi

A. Mwanzo 8:21 Mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake.

B. Waefeso 2:2-3 Kiasili mwanadamu ni mwenye dhambi.

C. Warumi 7:14-15 Mwanadamu ambaye hajakombolewa ni wa kimwili na anatawaliwa na dhambi.

D.Yeremia 17:9 Moyo usio na Mungu ni mdanganyifu na mwovu.

### III. Mahali Dhambi Hupatikana

A. Marko 7:20-23 Unajisi hutoka ndani ya mtu.

B. Mathayo 15:18 Dhambi hutoka ndani ya moyo wa mtu.

### IV. Wote Wametenda Dhambi

A. Warumi 3:23 Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

B. Warumi 3:9 Wayahudi na watu wa mataifa wote wamo dhambini.

C. 1 Yohana 1:8-10 Tukisema hatuna dhambi twajidanganya sisi wenyewe.

### V. Wote Watendao Dhambi ni wa Ibilisi

A. 1 Yohana 3:8a Atendaye dhambi ni wa Ibilisi.

### VI. Dhambi Huhusisha Mtu Kuamua Kukataa Mwangaza

A. Yohana 15:22-24 Mtu hupatikana kuwa na dhambi kwa kufahamu jambo na kukosa kuchukua hatua.

B. Yohana 9:41 Mtu hachukuliwi kuna ana dhambi ikiwa hana mwangaza wowote kuhusu dhambi.

C. Mahali ambapo hamna sheria yoyote basi mtu hachukuliwi kuwa mwenye dhambi.

### VII. Kujaribiwa Sio Dhambi

A. Mathayo 4:1 Yesu alijaribiwa na Ibilisi.

B. Waebrania 4:15 Yesu alijaribiwa kama tunavyojaribiwa lakini hakuwa na dhambi.

C. Yakobo 1:14-15 Tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi.

### VIII. Nguvu za Dhambi

A. Warumi 7:14-15 Katika mwili hamna nguvu za kushinda dhambi.

B. Warumi 7:23 Mtu wa kawaida yuko katika utumwa wa sheria ya dhambi.

### IX. Madhara ya Dhambi

A. Isaya 59:2 Dhambi hututenganisha na Mungu.

B. Yakobo 1:15 Dhambi huzaa kifo.

C. Yohana 8:34 Dhambi humletea mtu utumwa.

## X. Matokeo ya Dhambi

A. Yohana 8:21-24 Wanaokufa wakiwa katika dhambi zao hawawezi kuwa na Kristo.

B. Warumi 6:23 Mshahara wa dhambi ni mauti.

C. Zaburi 9:17 Waovu watatupwa jehanamu.

D. Mathayo 25:46 Adhabu ya milele.

E. Ufunuo 21:8 Kuhukumiwa hadi kwenye ziwa la moto.

## XI. Sadaka za Sheria Hazikuondoa Dhambi

A. Waebrania 10:1-4 Haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.

B. 1 Wafalme 8:46 Hakuna aliyeishi bila dhambi katika kipindi cha sheria ya Musa (Wahubiri 7:20).

C. Warumi 8:3 Sheria ilikuwa na udhaifu kwa ajili ya udhaifu wa mwili.

D. 1 Wakorintho 15:56 Uchungu wa mauti ni dhambi.

## XII. Ukombozi Utokanao na Utakaso wa Kristo

A. Zekaria 13:1 Unabii kuhusu utakaso wa dhambi.

B. Mathayo 1:21 Yesu alizaliwa ili kuwaokoa watu wake kutoka dhambini.

C. Warumi 5:10-12 Utakaso wa dhambi kupitia kwa Kristo.

D. 1 Yohana 4:10 Yesu ndiye kipatanisho cha dhambi zetu.

E. Waebrania 9:26 Yesu aliondoa dambi kwa kuyatoa maisha yake mwenyewe.

F. 1 Yohana 3:5 Yesu alikuja kuondoa dhambi.

## XIII. Maagizo ya Kutotenda Dhambi

A. Yohana 8:11 Enenda zako; wala usitende dhambi tena. (Yohana 5:14).

B. Warumi 6:12 Dhambi isitawale miilini mwenu.

C. 1 Wakorintho 15:34 Usitende dhambi.

## XIV. Nguvu za Kuishi Bila Kutenda Dhambi

A. 2 Wakorintho 5:17 Ya kale yamepita.

B. 1 Yohana 5:18 Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi.

C. 1 Yohana 1:7 Damu ya Yesu hutakasa dhambi zote.

D. Yohana 8:36 Mtakuwa huru kweli.

E. Warumi 6:13-18 Dhambi haitatawala.

F. Tito 2:11-12 Mwanadamu anaweza kuishi kwa utakatifu.

G. 1 Petero 2:21-22 Wakristo wanastahili kufuata mfano wa Kristo kwa kutotenda dhambi.

## MAANA YA DHAMBI

### AGANO JIPYA



1. Dhambi ni uasi dhidi ya sheria (1 Yohana 3:4).
2. Kila lisilo la haki ni dhambi (1 Yohana 5:17).
3. Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi (Yakobo 4:17).
4. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi (Warumi 14:23).

# SWALI na JIBU




**Swali:** Wengi wanaojiita Wakristo husema kwamba kila mtu hutenda dhambi "karibu" kila siku. Je, Mkristo anaweza kuishi bila kutenda dhambi?

**Jibu:**

Ndio. Sio tu kwamba Wakristo wa kweli wanastahili kuishi bila dhambi bali ni lazima wao kuishi bila kutenda dhambi. Lakini jambo hili haliwezekani kupitia kwa nguvu za mtu binafsi au uwezo wake. Kinachowezesha mtu kufanya hivyo ni nguvu zake Mungu kupitia Yesu Kristo ambaye ndiye humwezesha mtu kuishi bila dhambi. Neno "dhambi" ni neno linalotumika kwa njia nyingi na ni muhimu kutofautisha kati ya mtu kufanya makosa yanayofanyika wakati mtu anapokuwa akikua kama Mkristo katika sehemu tofauti za maisha yake dhidi ya mtu kufanya tendo la dhambi.

### WOTE WAMETENDA DHAMBI

"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;" (Warumi 3:23). Kila mtu ashawahi kuwa mwenye dhambi kwa maana hamna mtu yeyote mwenye uwezo ndani yake wa kushinda mwili wa dhambi. Sheria ya Musa ilitolewa ili kuonyesha wanadamu dhambi ni nini. Lakini hata wakati wa sheria ya Musa watu wa Mungu walifanya dhambi dhidi ya Mungu. Wao walitoa sadaka ambazo hazikuwa kamilifu na damu ya mafahali na mbuzi haikuondoa dhambi (Waebrania 10:4).

### SHERIA HAIKUWA KAMILIFU

"Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili" (Warumi 8:3). Yesu alikuja ulimwenguni na kumwaga damu yake, akafa, na akafufuliwa ili mwanadamu aweze kuwekwa huru kutokana na nguvu na utawala wa dhambi. "Na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7). Yesu alikuja "ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8). Yeye alifanyia wanadamu kile ambacho yeye hawangeweza kujifanyia chini ya sheria. Je, ikiwa mwanadamu angeendelea kuishi dhambini ndani ya Kristo kama alivyokuwa akiishi chini ya sheria haja ya damu ya Yesu ingalikuwa nini?

### YESU ANAOKOA KUTOKANA NA NGUVU ZA DHAMBI

Kuna maandiko mengi yanayodhihirisha kwamba mtu ambaye amezaliwa tena amekombolewa na kuokolewa kutokana na nguvu za dhambi. ". . . yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21). "Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema. Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha!" (Warumi 6:14-15). "Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki." (Warumi 6:17-18). Ni Dhahiri kwamba mtu anapotii Neno la Mungu kutoka moyoni mwake anasamewehe sio tu dhambi alizotenda mbeleni lakini pia anawekwa huru kutokana na nguvu za dhambi. Kiini cha "wokovu" ni kuokolewa kutoka dhambini.

### "ENENDA ZAKO WALA USITENDE DHAMBI TENA"

Yesu alimwambia yule mwanamke aliyepatwa katika uzinzi "Enenda zako; wala usitende dhambi tena." Maandiko pia yanafundisha kwamba "Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi" (1 Yohana 3:9). Mwanadamu amepata nguvu kupitia kwa damu na neema ya Kristo ili aishi bila kutenda dhambi: "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17). Kuna mabadiliko ya kimuujiza wakati mtu ameokoka kwa kweli kupitia kwa nguvu zake Yesu Kristo. Mkristo, mfuasi wa Yesu Kristo, anaweza kufuata mfano wake na kuishi bila kutenda dhambi (1 Petro 2:21-22). Wengi katika ulimwengu wa kidini wamefanya ukweli huu rahisi wa mafundisho ya Kikristo kuwa hafifu ili kutoa kisingizio cha wao kutenda dhambi.

### JE, KUFANYA MAKOSA NI DHAMBI?

Basi swali ni, "Unaposema kwamba kamwe Mkristo hatendi dhambi, ni kusema kwamba hatendi makosa yoyote?" Swali hili linazua umuhimu wa kuelewa maana ya dhambi. Mkristo anao uweza wa kugeuka na kuenda kinyume cha nguvu za Kristo na kurudia maisha yake ya dhambi lakini akifanya hivyo hatakuwa Mkristo tena. Kuna neema na nguvu za kuishi bila kutenda dhambi kama ilivyodhihirishwa kupitia kwa maandiko.

### KUKUA KWA MKRISTO

Ingawa sisi ni Wakristo tungali ni wanadamu. Basi wakati mwingine tutafanya makosa na tutapungukiwa na hekima. Sisi tumo safarini ya kukua

kiroho huku tukitafuta nguvu zaidi katika neema za Kristo na katika tunda la Roho wake. Maandiko yanatufundisha kwamba “Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo . . .” (2 Petro 3:18). Mkristo yumo safarini ya kukua katika mambo ya Mungu, safari ya kukua na kuzidi kuwa kama Kristo. Kuna wakati ambapo Mkristo hatakuwa na subira au furaha ambayo anastahili kuwa nayo. Hiyo siyo dhambi bali ni kusema kuna sehemu katika maisha yake ambayo inahitaji kutambuliwa na kuletwa kwa Bwana ili Mkristo huyo apate nguvu na neema zaidi.



### MOYO ULIOJITOLEA KWA MUNGU

Moyo wa Mkristo wa kweli una shauku isiyotingisika ya kumpendeza Mungu. Mkristo atajaribiwa kama Yesu alivyojaribiwa bila yeye kujitoa kutumikia dhambi (Waebrania 4:1). Kinyume cha vile ambavyo wengine wanafundisha mtu kupata majaribu sio dhambi. Mkristo hawezi kuzuia kila wazo ambalo linamwingia akilini, lakini kunazo nguvu kupitia kwa neema ya Mungu za kupigana na vitu ambavyo vinamhusisha mtu kutenda dhambi.

### DHAMBI HULETA UTENGANO

Dhambi ndiyo humtenganisha mwanadamu na Mungu (Isaya 59:2). Makosa hayamtenganishi mwanadamu na Mungu mradi tu yasitolewe vijisababu au kuchukuliwa kuwa ni matendo ya haki kutokana na moyo uliojaa kiburi. Sheria kuhusu tabia nzuri ilitolewa kwa njia ya sheria ya Musa. Kristo naye akatilia mkazo sheria hiyo ya tabia nzuri na hata viwango vyake akavifanya kuwa za juu zaidi kwa maana katika mahubiri yake pale Mlimani (Mathayo 5-7) Yeye hakushughulikia tu matendo ya mtu bali pia hali ya moyo wa mwanadamu.

### MAANA TOFAUTI ZA DHAMBI

Agano Jipya imetoa maana nne za kimsingi kuhusu neno dhambi – kile ambacho hutenganisha mwanadamu na Mungu. “Kila lisilo la haki ni dhambi” (1 Yohana 5:17). “Dhambi ni uasi dhidi ya sheria” (1 Yohana 3:4). “Yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi” (Yakobo 4:17).“Kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi (Warumi 14:23). Mtoto wa kweli wa Mungu huishi bila kufanya makosa dhidi ya maandiko hayo.

### NGUVU ZA KUKATAA MAOVU

Kuna nguvu kupitia kwa Kristo za mtu kuishi bila kwenda kinyume na sheria ya tabia bora ya Mungu kama ilivyofanyika wakati wa Sheria ya Musa. Mkristo ambaye anasema uongo, anaiba, anadanganya, na anatenda uzinzi hawi Mkristo tena. Na kusema kweli Mkristo wa kweli hata “hatataka” kufanya mambo hayo. Jambo hili linatokana na mtu kuwa na moyo safi mbele zake Mungu. Ni kweli kwamba kutakuwa na majaribu ya kusema uongo au kuiba, lakini kunazo nguvu za kuleta wazo hilo na kulifanya litii Mungu. Basi inakuwa kwamba Mkristo haendi kinyume na sheria na hafanyi tendo lisilo la haki ambalo limetokana na vitendo au malengo ya moyo wake.

Mkristo anayejua kile ambacho sheria ya Mungu inataka na anachagua kwa hiari yake mwenyewe kutotii huwa amefanya dhambi, kwa maana alijua jambo linalofaa kufanywa lakini hakuwa na shauku ya kuwa mtiifu. Tendo lenyewe pia halikutokana na imani. Mkristo anazo nguvu za kuishi kulingana na imani, huku akionyesha upendo na kutenda kulingana na sheria ya Mungu kuhusu tabia nzuri.

### WOKOVU HULETA MABADILIKO

Wokovu ndio huleta tofauti. Wokovu ndio ambao unawawezesha watu kuishi bila kutenda dhambi kwa sababu kuna neema na nguvu za kusema “la” kwa mambo yale ambaye yanatutenganisha na Mungu. Wokovu unawezesha watu katika uwanadamu wao kumkaribia Mungu zaidi na zaidi na kuendelea kuzaa matunda ya Roho. Upungufu wa kibinadamu sio dhambi bali ni hali ya kukua ambako mtu anaweza kufaulu na kukamilishwa kwa jinsi ambayo moyo wa mtu umedumishwa ukiwa safi na kuwa unakubalika mbele zake Mungu.

Neema ya Mungu inatosha kutudumisha na kutupatia ushindi hata katikati mwa majaribu ya maisha. Basi tumshukuru Mungu kwa uwezo wa kuishi bila kutenda dhambi! ■

**Je, Wajua?**

Neno Biblia linatokana na neno lingine la Kiyunani "Biblia" lenye maana ya vitabu.
Biblia ni kusanyiko la vitabu 66 ambazo zina sura 1189.
Agano la Kale lina vitabu 39.
Agano Jipya lina vitabu 27.
Mtume Paulo ndiye aliyeandika vitabu 14 vya Agano Jipya.
Agano la Kale liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania.
Agano Jipya liliandikwa kwa lugha ya Kiyunani.
Neno "agano" lina maana ya "mkataba" au "maagano."



*mengi zaida katika*
MTANDAO

*Tutembelee katika www.thegospeltruth.org Ili ujiandikishe na kupata jalida za kitambo.*


**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email
editor@thegospeltruth.org


UTAKATIFU KWA BWANA

**Neno Linalofaa kwa Msimu Huu**

## MKAPUMZIKE KIDOGO

*Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula.* —Marko 6:31

Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakieneza injili na kufanya kazi ya kujenga Ufalme wa Mungu. Muda si muda wakawa wamepokea habari ya kuuawa kwa Yohana Mtakatifu kwa njia ya kukatwa kichwa. Wanafunzi walikuwa na huzuni na pia walikuwa wamechoka na kukosa nguvu kwa sababu ya kazi ya kiroho waliyokuwa wakifanya na masumbufu ya kiakili ambayo huandama na kazi hiyo.



Basi Yesu akawaalika kutenga muda mbali na umati na mbali na kazi yake ili wapumzike na kupata nguvu mpya: "Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi" (Zaburi 103:14). Yesu alitambua umuhimu wa kuondokea masumbufu ya maisha na kutenga muda wa kupumzika.

Wahudumu wa kweli wa injili na wafanyi kazi wa injili hubeba mizigo mikubwa kwa ajili ya nafsi za watu wanaowazunguka. Wakati mwingine mahitaji na mizigo hiyo inaweza kumfanya mtu kukata tamaa. Mchungaji mmoja mzee wa kusanyiko letu alisema kwamba "wakati mwingine jambo la kiroho kabisa ambalo mtu anaweza fanya ni kulala usingizi kidogo."

Kwa kweli kazi ya Mungu inaweza kufaidika pakubwa wakati wahudumu wa Injili wanachukua muda wa kupumzika na kupata nguvu mpya. Wakati mwingi wahudumu wa injili huwa na msukumo mkubwa na kukazwa na mwito wa Mungu na mzigo wa kazi ambayo inahitaji kufanyika. Wengi wa wahudumu wamepatwa na masumbufu makubwa ya kiakili na hata kupoteza afya yao. Basi kuna haja ya kuondoka kwa siku kadhaa au wiki kadhaa kwenda mahali "jangwani" mbali na shughuli za maisha ya kila siku ili kupata kuhuishwa na kupata nguvu mpya. Wakati huu unaweza kuwa ni wakati wa kupata maono mapya na mielekeo mipya na hata wa kuweka malengo mapya kwa ajili ya kazi ya Bwana. Wakati watu wamepumzika akili zao huwa timamu na wanaweza kutimiza mambo makubwa zaidi. Basi ni jambo muhimu sana sisi kutambua kwamba kama ambavyo Bwana alifanya tunahitaji "kujitenga ili kupumzika kidogo." ■